GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZUU NO. **250** Shawwal-Dhl/Qadah **1446** AH April– **2025** Shahadat **1404** HS BEI TSH 800/=



JAMIA AHMADIYYA WATOWA ZAWADI YA EID- UL FITRI

UK. 08



Barua ya Seyyidna Ahmad[as] kuhusu Riba

Hazrat Masihi Aliyeahidiwa[as] aliandika barua moja kwa mfanyabiashara Mian Ghulam Nabi Sethi mnamo mwezi wa Aprili 1898. Ndani yake alitoa mwongozo kuhusu suala la riba.

Bismillahi Rahmani Rahim, Nahmuduhu wa Nusalli alaa Rasulihil Karim,

Mpendwa na Azizi wangu, Sheikh Ghulam Nabi,

Assalam o Alaikum wa Rahmatullah wa Barakatuhu

Jana nilipokea barua yako. Ninatarajia kwamba kwa sababu ya nia yako safi na uchaMungu Allah *(swt)* mwenyewe Atakufungulia mlango na kufanya wepesi. Hadi wakati huo yapaswa kufanya Istighfar kwa uvumilivu. Kwa maoni yangu mimi, matumizi bora ya pesa ya riba ni haya kwamba pesa ya riba ikipatikana usiitumie katika matumizi yako; bali uendelee kuikusanya pembeni na unapohitajika kulipa riba ulipe kwa pesa hizo. Na kama ukifikiri pesa hizi ni nyingi basi hakuna shida kutumia pesa hizo katika kazi ya dini isiyohusikana na matumizi ya mtu binafsi bali ifanyike kwayo kazi ya kueneza dini pekee. Mimi hapo awali niliwahi kutoa fatwa hii kwa wanajumuiya pia kwamba riba Aliyoiharamisha Allah ni kwa ajili ya matumizi binafsi. Ni haramu kwa mtu kutumia pesa ya riba kwa ajili ya kujikimu yeye mwenyewe na familia yake; au afanye matumizi ya chakula, mavazi na makazi, au atoe pesa hiyo kwa mtu mwingine ili yeye aitumie kwa ajili ya chakula au mavazi. Lakini si haramu kuitumia pesa hiyo kwa njia hii ya kwamba irudishwe kwa Mwenyezi Mungu bila kujipatia faida yoyote yaani itumike katika kueneza dini. Imethibitika na Kurani Tukufu kuwa Mwenyezi Mungu ni mmiliki wa kila kitu; na chochote kinachoelekea kwake kinakuwa safi isipokuwa zile mali zilizopokelewa kwa watu bila ridhaa yao kama vile za kuiba, za kunyang'anya na za kupora kwani mali hizo hazifai kutumika hata katika kazi za Mungu au za dini. Lakini mali iliyopokelewa kwa ridhaa inafaa kutumika katika njia ya dini ya Mwenyezi Mungu. Izingatiwe kwamba wakati huu sisi tunahitaji pesa kiasi gani kwa kulingana na wapinzani wetu wanaotoa machapisho dhidi ya dini yetu. Kana kwamba hii ni vita tanayopigana nao; katika hali hii hakuna shida katika kutoa pesa hizo ili kuisaidia Dini wakati wa vita. Hii ndiyo fatwa niliyoitoa. Yatosha kujiepusha na wanawake kwa kuinamisha macho yako bila kuwakodolea sana na endelea kufanya dua kwa Mwenyezi Mungu. Ni jambo la shukrani kwamba wewe daima umejaaliwa kutoa

UK. 03

Buriani Muhammad Iqbar Dar UK. 12 Buriani Muhammad Iqbar Dar

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

WAOGA

Hata wale ambao sio Waahmadiyya wanakiri kwa dhati kuwa watetezi na walinzi wa Islam kwa hivi sasa ni wafuasi wa Amir wa jeshi la Mtukufu Mtume Muhammad[saw] na Amir jeshi huyo ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Ni wanajeshi hodari na mahiri. Wakitokea uwanjani basi wale waoga ambao Shakespear katika Julius Kaisari anasema hufa vifo vingi kabla ya vifo vyao. Hukimbia na kutafuta mahali pa kujificha na hata juhudi hizo zao za kujificha zisizae matunda.

Padri Dale katika visiwa vya Unguja katika kutaka kuwasaidia Wahubiri wa Kikristo kuranda na kutamba kwamba Qur'an Tukufu (Allah Apishe mbali) si chochote, alitafsiri Qur'an Tukufu kwa Kiswahili miaka ya 1920. Dhamira yake kubwa ilikuwa ni kupaka matope dini tukufu ya Islam na kuonesha mafundisho ya Qur'an tukufu hayafui dafu mbele ya mafundisho ya Injili. Mkosi ulioje. Waislam wakapokea tafsiri hiyo kwa shangwe wakaiweka majumbani mwao wakiisoma asubuhi na jioni. Ama kweli Allah Asipokupa jicho la kuona huoni kamwe, na kama Hakukupa sikio la kusikia husikii abadani.

Ndugu zetu hawakuona udhalilishaji mkubwa uliofanywa na Padre Dale dhidi ya dini tukufu ya Islam. Ni jicho la mfuasi wa yule aliyetumwa kuirudisha Imani hata kama ingepaa kwenye nyota ya kilimia, yule ambaye alitumwa kufafanua maana za ndani za Qur'an Tukufu, yule ambaye alitumwa kuua nguruwe na kuvunja misalaba, wafuasi wake ndio waliweza kunusa harufu ya panya iliyokuwa imejificha nyuma ya tafsiri hiyo ambayo kwa hakika ilikuwa ni tafsiri kinzani. Kwenye tafsiri yake Padri Dale alikuwa ameficha matini ya Kiarabu ya Qur'an Tukufu. Kwa maana hiyo alimnyima msomaji wa tafsiri yake uwezo wa kupambanua usahihi wa tafsiri yake kwa kulinganisha na matini ya Kiarabu ya Qur'an tukufu. Hilo lilikuwa ni kosa kubwa la kuitafsiri Qur'an tukufu kwa Kiswahili bila kuonesha matini ya Kiarabu. Aidha kwenye tafsiri yake alijaribu sana kushambulia Tauhidi ya Mungu Mmoja na kujaribu kuthibitisha uungu wa Yesu. Jambo ambalo limekemewa sana na Qur'an Tukufu. Katika tafsiri yake pia alitafasiri majina ya Sura, jambo ambalo kwenye kanuni za kutafsiri halikubaliki, kwani majina huwa hayatafsiriwi. Majina ya sura zote za Qur'an tukufu yalikuwa yametolewa kwa hekima maalum na hivyo ilibidi kuyabakisha kwenye uhalisia wake bila kuyatafsiri. Pia Padri Dale kwenye tafsiri yake alijaribu kuonesha kuwa Qur'an tukufu inaunga mkono biashara ya utumwa, jambo ambalo ni kinyume kabisa na ukweli na uhalisia wa mafundisho ya Qur'an Tukufu na Islam kwa ujumla. Kwa ujumla tafsiri ya Padri Dale ilikuwa imejaa uchafu na tuhuma nyingi dhidi ya dini tukufu ya Islam.

Mwanazuoni Sheih Mubarak Ahmad alijibu shutuma zote na akaponda mafundisho dhaifu aliyojitia pambani kuyaeneza, akadhihirisha ubora na utukufu wa dini ya Islam. Bomu hilo kutoka mbinguni likamsaga adui tikitiki.

Hivi leo nenda kila Maktaba iwe Maktaba ya taifa, Maktaba za vyuo, Maktaba za mashuleni, kwenye maduka ya vitabu hutapata nakala hata moja ya tafsiri hiyo ya Padri Dale. Tumeulizia kutoka kwa waliochapisha tafsiri hiyo, jamaa zetu hao wamepatwa na ububu wa ghafla. Haipatikani mahali popote tafsiri hiyo na hiyo ndio maana sahihi ya ujaji wa Masihi na Mahdi kuondoa madoa yaliyoingia katika dini ya Islam. Kurejesha heshima ya Mtukufu Mtume Muhamamd (saw) na kuonesha bayana usahihi na ubora wa dini ya Islam.

Kazi nyingine iliyojitokeza katika shabaha hiyohiyo ya kujaribu kuponda mafundisho ya dini tukufu ya Islam ni kitabu cha 'Wana wa Ibrahim' kilichotungwa na Padri H. P. Anglars. Kitabu hicho ni kichafu katika maana halisi ya neno hilo. Katika kitabu chake Padri Anglars amejaribu kushambulia dini tukufu ya Islam na kutoa shutuma nyingi na tena amejaribu kuonesha humo kwamba Wakristo ndio Watoto wa Hadhrat Ibrahim na sio Waislam. Uchafu huo umesafishwa na Mwanazuoni wa Ahmadiyya sheikh Jamil Rahman Rafique katika kitabu chake cha 'Mwana Mkuu wa Ibrahim'. Kwa mara nyingine tena jitihada ilifanyika ya kutafuta angalau nakala moja ya kitabu cha 'Wana wa Ibrahim' lakini hatukufanikiwa.


Waahmadiyya tunaposema jihadi kwa hivi sasa hakuna, maana yetu ni hii kwamba jihadi ya upanga sasa imekwisha. Jihadi iliyobaki ni jihadi ya kalamu na kwa msaada wa Allah Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya inashinda katika kitali hii.



QUR'AN TUKUFU

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تُحِلُّواْ شَعَٰٓئِرَ ٱللَّهِ وَلَا ٱلشَّهۡرَ ٱلۡحَرَامَ وَلَا ٱلۡهَدۡيَ وَلَا ٱلۡقَلَٰٓئِدَ وَلَآ ءَآمِّينَ ٱلۡبَيۡتَ ٱلۡحَرَامَ يَبۡتَغُونَ فَضۡلٗا مِّن رَّبِّهِمۡ وَرِضۡوَٰنٗاۚ وَإِذَا حَلَلۡتُمۡ فَٱصۡطَادُواْۚ وَلَا يَجۡرِمَنَّكُمۡ شَنَـَٔانُ قَوۡمٍ أَن صَدُّوكُمۡ عَنِ ٱلۡمَسۡجِدِ ٱلۡحَرَامِ أَن تَعۡتَدُواْۘ وَتَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡبِرِّ وَٱلتَّقۡوَىٰۖ وَلَا تَعَاوَنُواْ عَلَى ٱلۡإِثۡمِ وَٱلۡعُدۡوَٰنِۚ وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلۡعِقَابِ

*Enyi mlioamini! Msivunje hishima ya alama za Allah wala ya mwezi mtakatifu, wala ya dhabihu, wala ya makoja yao, wala ya wale wakusudiao kwendea kwenye Nyumba Takatifu kutafuta fadhili na radhi za Mola wao. Na mtokapo katika Ihramu. basi windeni. Na uadui wa watu usiwashawishini kwa sababu waliwazuilieni Msikiti Mtakatifu ya kwamba mruke mipaka Na saidianeni katika wema na utawa. Wala msisaidiane katika dhambi na uasi. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.
(*Sura Almaidah aya .3)*



NUKUU YA HADITHI

Amesema Mtume[saw]: (Mwenye kumuondolea Muumini dhiki ya dunia, Allah atamuondoshea dhiki ya siku ya Kiyaamah, na anayemsahilishia dhiki, Allah atamfanyia wepesi mambo katika Dunia na Akhera,na Allah humsaidia mja maadamu mja anamsaidia ndugu yake. (***Sahih Muslim,Kitab uz zikri wa ddua.)***



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Yeye anasema. Kanuni tunayoifuata ni hii kwamba tuwe na huruma moyoni mwetu kwa ajili ya wanadamu wote. Kama mtu ye yote akiona nyumba ya jirani yake Baniani imepamba moto na hajitokezi kusaidia kuuzima moto, nasema kwa hakika kwamba mtu huyo si wa kwangu. Kama mfuasi wangu ye yote, baada ya kumwona mtu fulani, akijaribu kumuua Mkristo, hajitokezi kujaribu kumsaidia Mkristo yule, nasema kwa kweli kwamba mfuasi huyo hayumo kundini mwetu.
(Roohani Khazain Jal. 12, Uk. 28, Siraj-e-Muneer Uk. 26)

Kisha anasema.

Nawatangazia Waislamu, Wakristo, Mabaniani na Waarya, kwamba katika nafsi yangu mimi sina adui duniani. Nawapenda wanadamu jinsi mama mpendwa awapendavyo wanawe; bali kwa dhati zaidi. Mimi ni adui wa itikadi mbovu pekee, zenye kuhilikisha ukweli. Huruma kwa wanadamu wote ndio wajibu wangu. Kanuni yangu ni kutupilia mbali udanganyifu. Naukataa upagani, uovu, ubaya, dhulma na ufisadi. (Roohani Khazain Jal. 17: Arbaeen sehemu 1, Uk. 2

BODI YA UHARIRI

Msimamizi:	Sh.. Khawaja M. Ahmad - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri:	Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta:	Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji:	Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji:	Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:	1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga 2. Mahmood Hamsin Mubiru. 3. Sheikh Shahab Ahmad. 4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.

Barua ya Seyyidna Ahmad[as] kuhusu Riba

Kutoka uk. 01

mali yako katika kuisaidia dini. Wakati huu penye haja hii ni kazi ambayo kwa mujibu wangu mimi ni njia rahisi sana ya kumridhisha Mwenyezi Mungu. Hivyo, yapaswa kutoa shukrani kuwa Allah (swt) Alikujaalia uwezo na mimi ninaona kwamba daima uko mstari wa mbele katika kazi hii. Mwenyezi Mungu hutazama vitendo hivi naye Atatoa malipo. Mbali na hayo yapaswa kujishughulisha na dua na istighfar. Mambo mengine ni salama, Wassalaam.

Mimi mnyenyekevu,

Mirza Ghulam Ahmad, kutoka Qadian. 24 Aprili 1898

P.S. Simaanishi kwa kusema pesa ya riba kutumika katika kueneza dini kwamba mtu ajiingize maksudi katika biashara hii. Bali inamaanisha kuwa mtu akikabiliwa na hali kama ya kwako kwamba amepata pesa ya riba kwa sababu yoyote isiyoepukanika basi pesa hiyo inaweza kutumika kwa njia niliyoeleza na hivyo atapata thawabu pia.

Hazrat Mirza Bashir Ahmad[ra] alisema: Mimi ninatambua barua hii vizuri kwamba ni barua aliyoiandika Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as). Mambo muhimu yafuatayo yanapatikana kutoka katika barua hiyo.

1. Pesa inayopatikana kama riba inaweza kutumika kulipa riba. Ikiwa hali imebana sana na mtu akilazimishwa kutoa riba basi hii ndiyo njia nzuri kwamba pesa ya riba itolewe katika kulipa riba. Wafanyabiashara waislamu wasiopata kuepukana na riba kwa sababu ya hali ya dunia inayowazunguka wanaweza kufanya hivyo.
2. Pesa ya riba inatakiwa kuhesabiwa na kuwekwa mbali na pesa nyingine ili isichanganywe na pesa yako na pia iwe rahisi kuweka hesabu ya matumizi yake.
3. Pesa ya riba haiwezi kutumika kwa ajili ya matumizi binafsi wala isipewe kwa mtu mwingine kwamba yeye atumie kwa ajili ya matumizi yake binafsi.
4. Pesa ya riba inaweza kutumika katika kazi ya dini ambayo haihusiani na matumizi ya mtu binafsi kwa mfano kuchapisha vitabu, matumizi ya posta, na kadhalika.
5. Mali zinaweza kutumika katika njia ya dini ambazo ingawa haziruhusiwi kutumika kwa watu binafsi lakini hazijakusanywa bila kuwa na ridhaa ya watu; yaani mali zisizokusanywa kwa kulazimisha au kwa kudanganya jinsi inavyotokea katika wizi, uporaji, hiana na kadhalika.
6. Hali tete ya Uislamu na ya waislamu katika zama hizi inaunga mkono fatwa hii.
7. Haitakiwi kufanya hivi kwamba mtu ajiingize maksudi katika biashara ya kupokea na kutoa riba bali fatwa iliyoelezwa hapo juu ni katika hali ile tu ambayo kama kuna sababu isiyoepukika au mtu akipata pesa ya riba bila ya kutarajia.
8. Katika zama hizi kawaida ya kupokea na kutoa riba imeenea sana katika mambo ya biashara na kwa sababu yake hakuna biashara kubwa inayoweza kufanywa bila ya kushughulika na riba. Hii ni aina moja ya udhuru na kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa juu riba ya aina hii inaruhusiwa. Kwani Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alizingatia na akakubali udhuru wa Bwana Sethi aliyekuwa mfanyabiashara na aliyekabiliwa na hali kama hizi. Yaani anavyotaka Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as) ni kwamba mtu yeyote asifanye biashara kwa lengo la kupata riba. Hata hivyo, katika biashara yake akipata kupokea au kutoa riba basi hakuna shida; na fatwa hiyo imetolewa kwa kuzingatia hali kama hii. Kwa mujibu wa Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as) haitakiwi waislamu waache kufanya biashara au wajiwekee mipaka ya kufanya biashara ndogondogo tu zisizokuwa na changamoto za riba huku wakihofu kwamba watajihusisha na riba na isije wakaharibu uchumi wao kwa kulinganisha na watu wa dini nyingine.
9. Kwa mujibu wa fatwa hii benki zinaweza kuanzishwa kwa ajili ya ustawi wa waislamu na ndani yake -sawa na masharti yaliyoelezwa hapo juu- hakuna shida ya kufanya biashara ya kupokea au kutoa riba kama ni lazima kufanya.
10. Mtu anayepata pesa ya riba na kwa mujibu wa fatwa hii atatumia katika njia ya Mwenyezi Mungu atapata thawabu kwa Allah.
11. Agizo jingine lililoelezwa katika barua hii ni kuhusu kuonana na wanawake. Siku hizi wanapatikana wanawake wengi wasiozingatia hijabu na haiwezekani ujiepushe kikamilifu kuwaangalia. Baadhi ya wakati mwanaume anatakiwa kukutana na wanawake kama hawa. Hazrat Masihi aliyeahidiwa (as) alitoa mwongozo juu ya jambo hili kwamba mwanaume anagalau awe makini kiasi kwamba asiwakodolee macho bali ainamishe macho yake; na si ashindwe kuonana nao kabisa kwani hii ni aina mojawapo ya udhuru mbele ya wanawake. Hata hivyo, mwanaume anapaswa kumwomba Mwenyezi Mungu ili Amwepushe na mtihani wowote. Mimi nilipokuwa mtoto nilishuhudia kuwa Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as) aliinamisha macho yake akiwa anafanya mazungumzo na mwanamke asiyekuwa mwanafamilia wake kiasi kwamba ilionekana amefunga macho yake kabisa. Mimi ninakumbuka nilikuwa ninashangaa sana wakati huo kuwa kwa nini Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alifunga macho yake hivi lakini nilipokua nilielewa kwamba hekima yake ilikuwa ni hii.

Jambo jingine lililoelezwa katika barua hii ya Seyyidna Ahmad (as) ni hili kwamba katika zama hizi kwa sababu ya changamoto zilizoukumba Uislamu na waislamu kitendo bora kabisa ni kuitumikia na kuisaidia dini ya Uislamu na hakuna njia bora zaidi kuliko hii ya kumfikia Allah.

(Imetafsiriwa kutoka Kitabu cha Siratul Mahdi cha Hazrat Mirza Bashir Ahmad[ra], simulizi namba 442)

TANGAZO

UONGOZI WA LAJNA IMAILLAH TANZANIA UNAWATANGAZIA LAJNA NA NASRAT WOTE NCHINI KUWA IJTIMAI YA LAJNA IMAILLAH YA MWAKA 2025 ITAFANYIKA TAREHE 20,21 & 22 YA MWEZI JUNI KATIKA ENEO LETU LA KITONGA JIJINI DAR ES SALAAM.

KILA MWANATANZIMU ANAHIMIZWA KUMALIZA MCHANGO WAKE WA IJTMAI NA KUWEKA NIA YA DHATI YA KUHUDHURIA IJTMAI HIYO PAMOJA NA KUJIANDAA KUSHIRIKI KATIKA MASHINDANO YA KIELIMU NA MICHEZO.

PIA WAJUMBE WOTE WA SHURA KUTOKA MATAWI MBALIMBALI NCHINI WANAKUMBUSHWA KUJIANDAA NA SHURA YA KITAIFA ITAKAYOFANYIKA SIKU YA JUMAPILI YA MWEZI JUNI.

WASALAAM.

Athari ya dua

Hadhrat Maulana Ghulam Rasul Kudsi Rajekira sahaba wa Sayinda Ahmadas anasimulia: Kijijini kwetu aliishi kinyozi mmoja aitwaye Muhammad ud din. Ilipita karibu miaka ishirini tangu afunge ndoa, lakini hakujaliwa neema ya kizazi. Kwa kuwa familia yake ilikuwa na uhusiano mzuri na binamu yetu Hafiz Ghulam Husain Sahib na babake Hadhrat Mian Ilmud din Sahib, ndiyo maana kinyozi huyu pamwe na mkewe aitwaye Bi. Saidaan walikuwa wanawatembelea wazee hao wawili kwa ajili ya kuombewa na kupata hirizi. Lakini walipokosa kuona faida yoyote ya maombi na pagao ya muda mrefu basi wakakata tamaa kuhusu kupata kizazi. Katika zama hizo, kutokana na baraka za Uahmadiyya na Sayidna Ahmadas maombi yangu na athari zake ziliwikwa sana. Lakini kutokana na fatua za maulamaanakususiwakwetu na watu, hao hawakudiriki kunijia. Muhammad ud din kinyozi na mkewe Bi. Saidaan walikuwa wanasita kunijia mimi kwamba akijua Hafiz Sahib [binamu yangu], atakasirika. Lakini hali ya mume na mke wote wawili ilifikia hatua hii kwamba Bi. Saidaan akawaomba wazee hao wawili akisema: Kama hatuwezi kupata mtoto wa kiume, hakuna shida, basi azaliwe mtoto wa kike, tutaridhika na hilo tu. Hapo baba yangu mdogo Hadhrat Mian Ilmud din Sahib akamwambia: Mwende kwa kijana Ghulam Rasul na kumwomba awafanyie maombi kwani Mungu Anasikiliza sana maombi yake na kumjulisha kwa njia ya ufunuo. Saidaan aliposikia haya akasema: Kwanza naona aibu kumwendea Bw. Ghulam Rasul; la pili Hafiz Sahib akipata taarifa, lazima atanikemea kuwa kwa nini ulimwendea Mirzayi [Muahmadiyya] huyu kwa ajili ya kufanyiwa maombi, hivyo basi umwambie wewe mwenyewe kufanya maombi kwa ajili yangu na ufanye maombezi kwake kwa ajili yangu. Hazrat Mian Sahib akajibu: Sawa nitaongea naye lakini kuenda kwenu kwake ni muhimu mno. Halafu Mian Sahib akamleta Bi. Saidaan kwangu na kuniambia: Bibi huyu ameniambia mara kwa mara kwamba nikuombe kumfanyia maombi, hivyo umwombee.Nikajibu: Wakati mpo nyinyi mawalii na mzee kama Hafiz sahib, pana haja gani kuniambia miye Kafir kuwafanyia maombi? Bi. Saidaan akasema: Kama masheikh wamewakufurisha, unatulaumu kwa sababu gani? Kama tungekuwa tunawafahamu makafiri, tusingewajia ili kufanyiwa maombi. Hapo nikamwambia: Kama ni hivyo, basi dua yangu itakuwa tu kwa ajili ya ukweli wa Uahmadiyya ili kwa dua hii mkatimiziwa hoja. Na wakati viongozi wenu na wazee wenu wanawafanyia maombi na hirizi, matokeo ya maombi yangu yatatofautishwa namna gani? Yawezekana Mola Mkarimu kwa baraka ya Sayidna Ahmadas Akisikia dua ya mnyenyekevu huyu, Awajaalie mtoto, lakini nyinyi mkaanze kuyachukulia matokeo ya maombi ya wazee wenu badala ya Ishara ya ukweli wa Sayidna Ahmadas! Kwa kuyasikia haya, ami yangu Hazrat Ilmud din Sahib alisema kwamba athari ya maombi na amali zetu, wameshaona miaka mingi kuwa havijawasaidia chochote. Kama unao wasiwasi wowote, naweza kukuandikia ili kukubali kushindwa katika maombi na hirizi zetu. Hapo nikasema: Kama unakiri jambo hili basi kuanzia leo kama akizaliwa mtoto wa kiume au wa kike kwa Bi. Saidaan na Muhammad ud din ndani ya mwaka mmoja, kutakuwa ni alama ya ukweli wa Uahmadiyya. Wao walikubali jambo hili. Nami nikaanza kumwomba Mwenyezi Mungu. Ni maajabu ya kudra ya Mungu kwamba akazaliwa mtoto wa kike kwa kinyozi huyo ndani ya mwaka huo huo kutokana na rehema ya Mwingi wa rehema na baraka za Masihi wangu wa Qadian. Wanakijiji na watu wengine waliotuzunguka walipoona ishara hii kuwa kinyozi amejaaliwa kizazi baada ya miaka mingi ya kufungwa ndoa, walistajaabu mno. Lakini hata hivyo watu hao wenye bahati mbaya hawakuusogelea Uahmadiyya. Kisha binti huyo alipokua, watu hao - kwa sababu ya uovu wao na shari- wakaanza kunasibisha karama hii ya kuzaliwa kwa binti huyo na viongozi wao. Na wakaanza kumtangaza Hafiz Sahib hapa na pale. Nilipoona kufichwa kwa ukweli wenyewe, nikaudhika mno, na nikamwendea baba yangu mdogo na kumwuliza: Haya yote ni nini? Yeye akajibu: Mimi najua na kukubali kwamba hii ni ishara ya maombi yako na Imam wako, lakini majahili hao wananasibisha karama hii na mwujiza huu kwa Hafiz Ghulam Hussain kutokana na chuki na bughudha ya hali ya juu ya Uahmadiyya. Kisha nikamwambia Bi. Saidaan pia kwamba umeshuhudia ishara ya ukweli wa Uahmadiyya na unasikia madai ya watu kinyume chake, basi unaficha ushahidi wa kweli. Hivyo, kwa sababu ya heshima ya Uahmadiyya nasema kwamba kama akizaliwa tena mtoto kwako baada ya binti huyo, ufahamu kuwa binti huyo hakuzaliwa kwa maombi yangu, bali alizaliwa kwa sababu ya maombi ya asiye-Mwahmadiyya; pia kama binti huyo tangu leo akibaki hai hadi mwaka mmoja, utakuwa na ruhusa ya kuchukulia kwamba binti huyo alizaliwa kutokana na maombi ya asiye-Mwahmadiyya. Basi, hili ndilo jambo litakalokuwa upambanuzi baina ya dua ya Mwahmadiyya na asiye-Mwahmadiyya. Maajabu ya Mungu ni kwamba Bi. Saidaan alipofika tu nyumbani baada ya kusikia hayo, mara binti yake alianza kuugua, kisha akafariki ndani ya mwaka mmoja, na baada ya hapo wanandoa hao waliaga dunia bila kuwa na kizazi. فاعتبروا يا اولى الابصار. Shikeni nasaha enyi wenye busara. ***(mfasiri; khurram shahzad)***

BURIANI MOHAMMED IQBAL DAR SAHIB

Kutoka Uk 12

Kama alivyofanya Mshairi Tennyson naliuliza hilo chozi, chozi una ujumbe gani, chozi linaniambia ni msiba mkubwa kaondoka aliyetupa jina la Taifa letu na utambulisho. Kaondoka aliyekuwa na mapenzi ya dhati na Taifa hili, hatunaye aliyependa kusaidia na kusikiliza shida za wengine. Tumetengana kimwili na yule aliyesaidia masikini. Ametuaga aliyethamini Jumuiyya ya Ahmadiyya kuliko kitu chochote katika maisha yake. Chozi lile linanikumbusha kuwa udugu uliyoletwa na Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] una thamani kubwa kuliko udugu wowote ule. ……***itaendelea toleo lijalo, Inshallah.***

MAJIBU YA BAADHI ZA SHUTUMA/PINGAMIZI DHIDI YA SEYYIDNA AHMAD[AS] KUWA KWAKE IBN MARYAM

بسم الله الرحمٰن الرحيم

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ آمَنُوا اِمْرَأَةَ فِرْعَوْنَ إِذْ قَالَتْ رَبِّ ابْنِ لِي عِندَكَ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَنَجِّنِي مِن فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهِ وَنَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهِ مِن رُّوحِنَا وَصَدَّقَتْ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَكُتُبِهِ وَكَانَتْ مِنَ الْقَانِتِينَ

"Na Allah amewapigia mfano walio amini mfano wa mke wa Firauni pale aliposema: Mola wangu Mlezi! Nijengee nyumba yako katika Pepo, na uniokoe na Firauni na kazi yake, na uniokoe na madhalimu. watu." "Na mfano wa Maryamu binti Imran aliyelinda utupu wake, na tukampulizia roho yetu, na akayatimiza maneno ya Mola wake Mlezi na Vitabu vyake, kwani alikuwa miongoni mwa watiifu." (Al-Tahrim 66: 12-13)

Katika mameno haya waaminio wanafananishwa na mke wa Firauni Alijitafutia maisha ya peponi, ukaribu na Mwenyezi Mungu. Vilevile waaminio wanafananishwa na Maryam Bint Imran. Aliyejilinda tupu yake na alipokea ufunuo wa Mwenyezi Mungu na kusadikisha ukweli wa mafundisho ya Allah na vitabu vyake. Alijithibitisha kuwa mmoja wa watumishi watiifu sana wa Mwenyezi mungu hapa waaminio wanaelekezwa kuwa ni wa namna mbili.

Aina iliyo mfano wa mke wa Firauni, na aina iliyo mfano wa Maryam. Ni dhahiri ya kuwa kwa akali aina moja ya waaminio ni ya mfano wa Maryam. Hivyo, kama aliyeahidiwa anaitwa mwana wa Maryam, inaweza kuwa ina maana kuwa huyo Nabii aliyeahidiwa, ataanzia na hali ya mfano wa Maryam, na kwa kukua katika hali hii , atafika hali ya mfano wa Issa[as] . inaweza kuwa na maana ya kuwa maisha ya awali ya Nabii aliyeahidiwa kufika mara ya pili yatakuwa matakatifu na yasiyo na dosari kama vile Maryam alivyokuwa mtakatifu na asiye na hila , alafu maisha yake ya baadae yawe sawa na ya Issa Ibn Mryam. Nabii Isa[as] alipata msaada kwa roho takatifu hivi ndivyo atakavyokuwa huyo Nabii aliyeahidiwa kufika kwa mara ya pili. Maisha yake yote yatapita katika kuthibitisha ukweli na kuleta islahi duniani.

Inasikitisha ya kuwa maulamaa wa wakati wetu hawafikiri kwa makini sana maneno ya kurani Tukufu. wamejipigia marufuku kuzamia maana yake. Ndio sababu, wanakosa ule uzuri na fadhila *iliyochini ya uso wa maneno matakatifu*. Lakini masheikh hao wangesoma maandishi ya masufi wa zamani wa kiislam, {maandishi yenye msingi wa Kurani Tukufu na sunnah za manabii wa zamani}, wangeliona ukweli.

Shekhe Shahaab-ud-din Suhrawardi, kataja mfano mmoja wa walii wa kiislam aliye andika yanayohusiana na madhumuni hii, anasema katika kitabu chake Awarif-ul-ma'aarif ya kuwa uzazi ni wa namna mbili: ''uzazi wa kimwili na uzazi wa kiroho. Akisaidia maelezo haya walii mkubwa huyu anaendelea kumtaja sio mtu mwingine bali Issa[as] mwenyewe. Shekhe anaandika:-

''Murid ni sehemu ya Sheikh, kama vile katika uzazi wa kimwili, mtoto ni sehemu ya baba. Murid anazaliwa kimethali katika maana aliyoiyeleza Issa[as] aliposema kuwa hakuna mtu atakaye ingia katika ufalme wa mbingu mpaka azaliwe mara ya pili. Uzazi wa kwanza unafungamanisha mtu na dunia hii, na uzazi wa pili unamfungamanisha mtu na ulimwengu wa kiroho. Na fundisho hili limo ndani ya Qur-an tukufu pia.

وَكَذَٰلِكَ نُرِي إِبْرَاهِيمَ مَلَكُوتَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلِيَكُونَ مِنَ الْمُوقِنِينَ

''Na hivyo, tukamwonesha ibrahim ufalme wa mbingu na ardhi, na ili awe miongoni mwa wenye yakini.''{6:76}.

Hivyo, kwa maoni ya shekhe Shahaab-ud-din kila mwanadamu anapata uzazi wa kiroho. Kwa kusaidia maoni haya anataja aya ya Kurani Tukufu na maneno ya nabii Isa a.s aliyoonelea kwamba uzazi wa kiroho ni wa lazima kwaajili ya maendeleo ya kiroho ya mwanadamu. Kwanini uzazi huu wa kiroho usiwezekane au uwe shida kwa Masihi aliyeahidiwa a.s ambaye ndiye mfano wa Nabii Isa[as].

Wanaanza kushangaa maana yake. Je, wanasahau kuwa mtu anayefanya vyema katika wema wa kutoa sadaka anaitwa kwa tamathali Hatam wa Tay, mtu mwenye akili za kifalsafa anaitwa Tusi, mtu anayeonyesha uwezo wa kufikiri kwa njia ya kiutetezi anaitwa Razi? Kwa nini basi kuleta shida yoyote kuhusu jina Ibn Maryam? Ikiwa jina Ibn Maryam ni jina la mtu anayejulikana, je, Hatam, Tusi, na Razi siyo majina ya watu wanaojulikana? Ikiwa, kwa kutoa majina haya kwa watu wengine hakuna mtu anayeingizwa mkenge kufikiri kuwa watu hawa ni Hatam, Tusi, au Razi wa asili, je, kuna yeyote anayepaswa kufikiria kuwa, wakati Yule Aliyeahidiwa anaitwa Isa Ibn Maryam au Yesu, mwana wa Maryam, lazima inamaanisha Yesu yule yule, mwana wa Maryam, ambaye alitokea duniani miaka 2000 iliyopita? Na bado kuna tofauti kati ya majina Hatam, Tusi, na Razi na jina `Mwana wa Maryam'. Ya kwanza kila moja limekuja kuwa na maana moja dhahiri, lakini jina Maryam limetumika kuelezea hali ya kiroho na Quran Tukufu yenyewe inasema:

وَضَرَبَ اللَّهُ مَثَلًا لِّلَّذِينَ آمَنُوا اِمْرَأَةَ فِرْعَوْنَ إِذْ قَالَتْ رَبِّ ابْنِ لِي عِندَكَ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَنَجِّنِي مِن فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهِ وَنَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهِ مِن رُّوحِنَا وَصَدَّقَتْ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَكُتُبِهِ وَكَانَتْ مِنَ الْقَانِتِينَ

"Na Allah amewawekea mfano wale wanaoamini mfano wa mke wa Firauni aliposema, 'Mola wangu! Nijengee nyumba kwako katika Bustani na uniokoe na Firauni na kazi zake na uniokoe na watu wenye kudhulumu." "Na mfano wa Maryam, binti wa Imran, aliyelinda usafi wake; hivyo tukampulizia ndani yake kutoka Roho yetu na akatimiza kwa nafsi yake Maneno ya Mola wake na Vitabu Vyake, kwa maana alikuwa mmoja wa watiifu." (Al-Tahrim: 12-13)

Katika lugha zote za dunia, neno linalotumika kuelezea harakati za mtu kutoka mahali pamoja hadi jingine ni tofauti na neno linalotumika kuelezea harakati za kurudi kutoka mahali pa pili hadi pa kwanza.

Ikiwa mtu anahama kutoka sehemu A hadi sehemu B, inasemekana kwamba anaenda kutoka sehemu ya kwanza hadi ya pili. Hata hivyo, baada ya kufika sehemu B na kurudi A, mtu huyo hachukuliwi kama anaenda sehemu ya kwanza bali anarudi huko. Vivyo hivyo, katika lugha ya Kiarabu, kwenda kutoka sehemu moja hadi nyingine huitwa Nuzool نزول, wakati kurudi kutoka sehemu ya pili hadi ya kwanza huitwa Ruj`u رجوع.

Inasadikiwa kuwa Hazrat Isa[as] alipaa mbinguni na atashuka duniani katika siku za mwisho. Kulingana na kanuni ya kiisilamu iliyotajwa hapo juu, kurudi kwa Hazrat Isa[as] kutoka mbinguni hadi duniani kungepaswa kuelezwa kwa Kiingereza kama "Return" na kwa Kiarabu kama "رجوع". Kinyume chake, katika Ahadith, popote ambapo kuja kwake katika siku za mwisho kunatajwa, neno "Nuzul نزول" limetumika badala ya neno "Ruju`u رجوع".

Hata hivyo, mtu anapaswa kukumbuka kuwa kulingana na imani ya wasio-Ahmadiyy yeye haji tu kutoka mbinguni hadi duniani bali "anarudi" kwani, inavyodhaniwa, alipaa kutoka duniani kwenda mbinguni.

Mifano isiyo na idadi kutoka lugha nyingi inaweza kutolewa kuunga mkono kanuni hii kwamba kurudi kwenye sehemu ya asili ya kuhamia kunaitwa 'kurudi رجوع'. Mfano wa aina hiyo kutoka katika fasihi ya Kiislamu unathibitisha kanuni hii, siyo tu kisarufi bali pia hutoa uthibitisho wa kimaandiko. Ni dhahiri kutoka kwa kauli ifuatayo ya Hazrat Umar(ra), hasa neno analotumia wakati wa kifo cha Mtume Mtukufus.a.w. kwamba neno linalotumika kwa kurudi ni Ruju`u na siyo Nuzool. Katika kauli hii Hazrat Umar(ra) hasemi kwamba Mtume Mtukufus.a.w. atakuja (atashuka) baada ya kukutana na Mola wake, kama Hazrat Musa[as]. Anachosema ni kwamba Mtume Mtukufu[saw] atarudi kama Hazrat Musa[as] alivyorejea.

ان رجالا من المنافقين يزعمون أن رسول الله ﷺ قد توفي، و ان رسول الله ما مات، ولكنه ذهب الى ربه كما ذهب موسى بن عمران، فقد غاب عن قومه أربعين ليلة، ثم رجع اليهم بعد أن قيل مات، ووالله ليرجعن رسول الله ﷺ كما رجع موسى، فليقطعن أيدي رجال و أرجلهم زعموا أن رسول الله ﷺ مات.''(السيرة النبوية لأبن أسحٰق جلد 2-1، ص-713، السيرة النبويه لأبن ہشّام جلد- 4، ص-306)

Tafsiri: Baadhi ya watu miongoni mwa wanafiki wanasema kwamba Mtume Mtukufu s.a.w amefariki. Hakika, hajafariki bali ameenda kwa Mola wake kama Musa[as] mwana wa Imran alivyokwenda, na alikaa mbali na watu wake kwa muda wa siku arobaini. Kisha alirudi na kisha akafa. Naapa kwa Mungu, Mtume[saw] hakika atarudi kama Musa[as] alivyorejea na kukata mikono na miguu ya wale wanaosema kwamba amefariki.

Allah anasema katika Qur`an Tukufu:

انظُرْ كَيْفَ نُصَرِّفُ الآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَفْقَهُونَ

"Tazama jinsi tunavyoeleza Aya kwa njia mbalimbali ili wapate kuelewa!" (6:66).

Itaendelea toleo Lijalo

Bustani ya Washairi

KUMI LA TATU

Salamu ndugu malenga, Hodi kwako tunabisha,
Mimi na Ami wa tanga, Jambo tunalifikisha,
Utufichulie kunga, Malumbano yasokwisha,
Kumi la tatu ni bora, zaidi ya yalopita?

Twahofia kutobanga, Hekima kuipindisha,
kujitwalia ujinga, Fikhi kuzibabaisha,
Bidaa humo kujenga, Muradi kuuyumbisha,
Kumi la tatu ni Bora, zaidi ya yalopita?

Ami abisha kilonga, Itikafu kuonyesha,
Lai qadri ajenga, Hoja kututaabisha,
Moto mbali kututenga, neema zisizokwisha,
Kumi la tatu ni bora, Zaidi ya yalopita.

Mimi kwako nimetinga, Fumbo kumuelimisha,
Aelewe kinaganga, Hekima aloridhisha,
Mola alipozitenga, Dua nakutufundisha.
Si ni kweli zipo sawa, Kumi tatu za swaumu!???

'RABBI'

Rabbi akishakubali, akaridhi Mola wangu
Jingine hapo sijali, bora kakubali Mungu
Alipendalo Jalali, hilo maridadi kwangu
Nitashika hilo hilo hadi siku ya hesabu.

Na Mahmood Hamsin mubiru (Wamamba)
Kiwalani –Migombani, Dar es salaam.

MUNGU WETU HANA DINI

Ndugu zangu habirini, wenye dini wapagani
Sikio niazimeni, mungu wetu hana dini
Chuki sababu ya dini, hutookoka motoni
Mapenzi yawe kwa wote, bila chuki kwa yeyote.

mmoja ulimwenguni, ndiye muumba wa wote
Mungu wa duniani, sayari na nyota zote
Mungu wetu hana dini, habagui vyake vote
Vilivyoko aridhini, hata vya mbinguni vyake.

Vyakuvila aridhini, wanyama nayo mimea
Hewa maji duniani, kila kitu cha tumia
Mungu wetu hana dini, tuache kujibagua
Kila kitu limwenguni, mahitaji akatoa.

Ubora ulimwenguni, binadamu akapewa
Atawale vya mbinguni, na akili akapewa
Mungu wetu hana dini, tutumie tulopewa
Sigombane kisa dini, utu ukapuuziwa.

Akaiweka na dini, Ili tuweze mtambua
Dunia iwe amani, kila kiumbe tulia
Mungu wetu hana dini, kazi kwetu kumjua
Dini hasa ni amani, salama kuwa dunia.

Utulivu duniani, upendo na usalama
Ndilo hasa dhumuni, yakujitendea wema
Mungu wetu hana dini, humpenda alomwema
Una dini mpagani, wengine wawe salama.

Acha nifike mwishoni, akili mekufunguw,
Mungu wetu hana dini, acheni kujibaguwa
Kama kafiri kwa dini, kimaisha takutowa,
Tupendane bila dini, kituacha metugawa

Masihi Omary Stambuli

MAJINA YA ALLAH (99)
SIFA ZA RAHMAN

Zifuatazo ni sifa, kwa majina za vutia,
Kwazo hujiziba nyufa, za shaka mola dhania
Pia hujaza nadhifa, za roho na mwili pia
Mola wetu asokufa, Kwa sifa ametimia.

1.Kwa allah ninaanzia, sifa zote limebeba
Upweke la oneshea, hakuna wakuliiba
Mwenye kujitegemea, mkwasi asiye haba
Viumbe watajifia, ye milele atakaa

2. Rahmani mwingi rehema, ulimwenguni kajaza
Hata kabla umba mama, mahitaji lieneza
Toka kile cha kulima, hadi cha bahari jaza.
Ya mama yote rehema, kwake ni moja ya mia.

3. Rahimu Wa ukarimu, mfano wake hakuna
Lo wapa vya kujikimu, viumbe wakajivuna
Wale alowarehemu, malipo wanayavuna
Jema wanapohudumu, thawabu huwapatia

4. Maliki wetu mfalme, sisi kwako tegemezi
Ukubwa Wa wako falme, mipaka hijitokezi
Uwezo Wa yako falme, ni ule toka Wa enzi
Mwenye nguvu mfalme, humpa humtakae

5. Qudusi ni mtukufu, kasoro zimemwepuka
Mfano Zile za ufu, au uchovu mshika
Au usahaulifu, au usingizi shika
Siku Zote mtukufu, heshima mwenye stahiki.

6. Salam mwenye Amani, viumbe kuwa tuliza
Japo wamo rehemani, hawaachi mchukiza
Hushindania dhambini, visasi kujilipiza
Yeye hutoa Amani, akhera dunia pia.

7. Al muumin manani, imani mwenye kutoa
Uwatia salamani, wale alowaridhia
Huchunga zao imani, shetani sije wazoa
Kwa salama na imani, wapendwa wake walea

8. Muhaymin mtunzaji, Wa kila alichoumba
Na pia mwangaliaji, mlinzi Wa avoumba
Kwa qudra ni mwendeshaji, namna alivyoumba
Kianzacho mlindaji, mwisho hukifikishia.

9. Al Aziz mwenye shani, Nguvuze si za mfano
Huoni wake mwishoni, eti shindwa mashindano
Awekalo ukumbini, halitoki kwa mkono
Wala kwa Nguvu ya jini, bila yeye kuridhia.

10. Jabbar Nguvu kajaa, hufanya analotaka
Kilichojivunjikia, kwake hutengenezeka
Kilichojipungukia, kwake hukamilikika
Nguvuze Zilizojaa, hakuna chakupimia

11. Mutakabbir mkubwa, ukubwa wote ni wake
Vyadhihirisha ukubwa, vile vitokavyo kwake
Kila kitu cha ukubwa, yeye yuko juu yake
Mutakabbir mkubwa, hana wakufanania.

12.khaliq mwenye kuumba, ameumba kila kitu
Vyakuoneka kaumba, toka kwa kisicho kitu
Visooneka kaumba, toka kwa kisicho mtu
Ni mbora kuumba, huumba licho ridhia.

13.baari mtoa uhai, viumbe wapa maisha
Hukadiria uhai, na kipindi cha kuisha
Mmiliki wa uhai, huleta wa kuondosha
Baari mtoa uhai, viumbe na mimea.

14.al muswawwiru huunda, za viumbe zao sura
Atakalo hulipinda, mraba au duara
Huchagua nalopenda, endane na ile sura
Umbile analohunda, fanane yake tabia.

15.kwa jina al ghafar, husamehe na kubali
Madhambi yalodhahiri, na hata yale yasiri
Zenye kujaa bahari, hata za kwenye bakuli
Husamehe walokiri, epusha adhabu kali.

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

Baba

Tunu ilosaulika, vinywani kutamkwa
Juhudi walizoweka, thamani kutopewa
Ubaya kuwapachika, uzuriwo fahamiwa
Baba nazungumzia, thamani yake apewe

Mwana kwa mama twajua, tangu kale wagandana
Nyonyo akimpatia, mgongoni kibebana
Bembelezwa akilia, chakula kupatiana
Baba nazungumzia, thamani yake apewe

Baba likutafutia, mama unojivunia
Chakula awaletea, upate chakunyonyea
Viraka ajivalia, kwenu awanunulia
Baba nazungumzia, thamani yake apewe

Adimu kukaa naye, rizikiyo kuisaka
Muda ukiwa nayeye, uchovu umemshika
Tamwona asinziye, au mawazo mshika
Baba nazungumzia, thamani yake apewe

Ukali tamsikia, kipigo utachezea
Lengo ni kukuzuwia, kuinyoosha tabia
Yasomana yaachia, yamsingi kazania
Baba nazungumzia, thamani yake apewe.

Mshairi wetu

KULISHA

Halishwi yeye hulisha, Rabbi mtoa riziki
Sifa hino inatisha, nani anaimiliki?
Nani aweza kuvisha, lau lapa la kaniki?
Udongo walima pamba, nani kautengeneza?

Na Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba
Kiwalani - Dar es salaam.

MPANGAJI

Binadamu mpangaji, hino nyumba ya wageni
Hakuna alo mwenyeji, wa kudumu duniani
Moja la kutufariji, sote tumo safarini.
Vipi upate sururi, Safari bado ni ndefu?

Safari bado ni ndefu, imejaa mitihani
Umesambaa uchafu, mijini na vijijini
Watupa kichefuchefu, kutapika majiani
Penye donda tunaweka, msumari wenye moto.

Msumari wenye moto, ndiyo twaweka mwilini
Huo msiba mzito, kujipeleka motoni
Simulizi sio ndoto, tunahusudu shetani
Na furaha yake moja, ya sisi kuangamia.

Ya sisi kuangamia, kuiacha yetu dini
Mafunzo aliyotoa, yamo kwenye Qur'ani
Mabegani yametua, hatujali asilani
Vipi utayasafisha, machafu tunayoona?

Machafu tunayoona, ni nani huyo ni nani
Kwa marefu na mapana, ayaondoe njiani
Ili itoke laana, ya kumuasi Manani.
Nani anao uwezo, ghairi yake Rasuli


Ghairi yake Rasuli, hatupati afuweni
Twamshukuru Jalali, kaleta wa Qadiani
Hakimu mwenye adili, haraka tujiungeni.
Na Jamaat ya mbinguni, tuupate utulivu

Na Mahmood Hamsin Mubiru –Wamamba
Kiwalani - Dar es salaam.

Hadithi ya Confucius Two--
Kurudishiwa Farasi

Siku moja Confucius alitoka kwa ajili ya safari. Wakati alipokuwa akipumzika njiani farasi wake akakimbia na kula katika shamba la mkulima. Mkulima alipomuona farasi alikasirika sana. Akamkamata na kumfunga pamoja na mifugo yake.

Confucius alihuzunika sana kujua kilichotokea. Alikuwa na mwanafunzi wake Zi Gong ambaye alikuwa msomi hodari na mhutubu mahiri. Mwanafunzi huyu aliomba ruhusa kwa mwalimu wake ili aende kwa mkulima huyo na akarudishe farasi wake.



Zi Gong akaenda na akamwomba mkulima kwa adabu sana. Mkulima huyo akiwa amekasirika hakujali nafasi ya Zi Gong wala heshima ya Confucius na akakataa kabisa kurudisha farasi. Zi Gong alijaribu tena kumwomba kwa adabu lakini aligonga mwamba. Zi Gong akavunjika moyo na akarudi kwa Confucius akilalamika.


Confucius akaelewa kosa lake la kumruhusu Zi Gong kwenda kuzungumza na mkulima. Akasema: Zi Gong wewe ni msomi mwenye ujuzi na yeye ni mkulima asiye na elimu, nyinyi hamwongei lugha moja. Nisingalikuruhusu wewe kutekeleza jambo hili. Ulitumia hoja ambazo hazikueleweka kwa mkulima ndio maana mlishindwa kuelewana. Mazungumzo yenu hayakuleta faida.

Lakini sasa ninamwagiza mfanyakazi wangu anayefuga farasi zizini kwenda kuongea na mkulima huyo. Mfanyakazi akaenda kwa mkulima na akamwambia, wewe unalima hapa mashariki na mimi ninakaa magharibi hatujawahi kufahamiana lakini mashamba yetu yanafanana. Farasi huyu alishindwa kujua hili ni shamba lako au shamba langu. Hapo mkulima akamwelewa na akamsamehe kwa kurejesha farasi.

Maoni ya Mwandishi:

Baadhi ya watu wanaonesha elimu na uzoefu wao pasipokuwa na nafasi. Ingawa wana elimu nyingi kuitumia katika mahali panapofaa ni muhimu sana. Ukitaka hoja yako ikubaliwe inabidi uieleze vizuri kwa yule anayekusikiliza. Wahenga walivyosema, ndege wa aina moja huruka pamoja. Watu huwa hawapendi kuwakubali watu wanaojifanya kuwa tofauti na wengine. Hivyo kiongozi hodari humchagua mtu anayefaa kufanya kazi sawa na nafasi husika.

Unganisha Nukta kupata Mchoro



JIFUNZE KUPIKA KISAMVU CHA NAZI

MAHITAJI

- Kisamvu fungu kubwa 1
- Nazi 1
- Vitunguu maji 2
- Vitunguu thoum kiasi
- Mafuta kidogo
- Chumvi kiasi



JINSI YA KUPIKA KISAMVU

1• Kichambue kisamvu, kioshe, kisha ukitwange kilainike. Inapendeza ukikitwanga ukiwekee vitunguu swaumu na pilipili kama unatumia.

2• Kichemshe mpaka kiive, kikauke

3• Bandika sufuria, weka mafuta, yakipata moto weka vitunguu kaanga, kisha weka vitunguu swaumu, tia mboga yetu. Weka chumvi na tui zitozito.

4. Wacha ichemke hadi tui likauke, mboga tayari.

#NB Wengine hawatii Mafuta wanaweka kila kitu baada ya kuchemsha.
Unaweza kuweka na kunde mbichi wakati unachemsha kinakuwa kitamu sana.

JAMIA AHMADIYYA WATOWA ZAWADI YA EID- UL FITRI

Kutoka Uk> 01

Kama ilivyoada, wanatawi wa Jamia Ahmadiyya kila mwaka katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani kabla ya siku ya Eid huwakumbuka majirani na wenye uhitaji maalum kwa kuwapatia zawadi ya chakula (mchele na unga wa mahindi). Mwaka huu (2025) zoezi hilo lilifanyika siku ya Jumamosi tarehe 22, March 2025 sawa na tarehe 21 Ramadhani 1446 A.h, katika ukumbi wa chuo Kihonda Morogoro.



Mgeni rasmi katika Hafla hiyo ya ugawaji wa zawadi alikuwa ni Mkuu wa wilaya ya Morogoro Mjini, Mh Musa kilala. Hafla ilikuwa chini ya Mwenyekiti Maulana sh. Khawaja Muzzaffar Ahmad Sahib Amir na Mbashiri Mkuu hapa Nchini.

Halfla ilianza majira ya saa nne na nusu asubuhi kwa usomaji wa Quran Tukufu iliyosomwa na bwana Shadad Said na kufuatiwa na Qasida ya kiarabu iliyosomwa na bwana Abusidiq A. Pembe na kufuatiwa na hotuba ya utambulisho wa jumuiyya ya Waislamu wa Ahmadiyya iliyosomwa na Mwalimu Hussein Omari Mpenda Sahib.

Baada ya utambulisho huo, ilifuata hotuba fupi juu ya mafundisho ya Seyidna Ahmad a.s na jinsi alivyotekeleza katika Maisha yake. Hotuba hiyo ilitolewa na mwalimu Shamuni Juma sahib.

Kisha zilifuata salamu za shukrani kutoka kwa Mheshimiwa diwani wa kata ya kihonda kaskazini kwa niaba ya muheshimiwa diwani wa kata ya Kihonda Maghorofani- Ambaye alikuwa na dharura. Katika salamu zake Muheshimiwa diwani alishukuru sana Jamaat kwa utaratibu huo mzuri wa kuwakumbuka Maijirani na wahitaji Mbalimbali.
Baada ya salamu za Mheshimiwa diwani, lilifuata zoezi la kutambulisha wageni, kazi hiyo ilifanwa na Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhat sahib Naib Amir na mkuu wa chuo Jamia Ahmadiyya Tanzania.


Baada ya hapo ilifuata Hotuba ya Mgeni rasmi, katika Hotuba yake alianza kwa kunukuu hadithi ya Mtume Mtukufu s.a.w isemayo '' hata amini yeyote kati yenu mpaka ampendelee nduguye kama anavyojipendelea nafsi yake. ''kisha akaipongeza Jamaat kwa kuwakumbuka wahitaji katika kipindi hiki cha sikukuu. Na akazitaka taasisi zingine kuiga mfano huu Mzuri.

Kisha ilifuata hotuba ya Amir Sahib, naye baada ya Tashahud alianza kwa kutoa shukran Kwa Allah na kwa wageni wote waliohudhuria katika hafla hiyo. Kisha alipongeza idara ya Jamia kwa kuandaa Mpango huu mahsusi wa kuwakumbuka wenye shida mbalimbali. Akaongeza kusema kwa kuwajali viumbe wa Mwenyezi Mungu ni jambo zuri na linavuta karibu zaidi rehema za Allah. Siku ya qiyama Mwenyezi Mungu atamuuliza Mja wake akisema, ewe mja wangu mimi nilikuwa nina njaa hukunipa chakula, nilikuwa na kiu hukunipa maji, mja atajitetea akisema, wewe ni mkwasi niliniulikosa chakula, maji, mavazi na kadhalika? Allah atasema je hukumuona mja wangu Fulani aliyekuja kwako kuomba msaada? Kama ungemsaidia yeye ungeni kuta kwake- Alisema Amir Sahib na kuwahimiza watu kujenga na kudumisha utamaduni wa kuwasaidia wenyeuhitaji.

Baada ya hotuba yake, Amir sahib aliongoza maombi ya kimya na kasha zoezi la kugawa zawadi.
Pamoja na wahitaji mbalimbali, zawadi hizo pia ziliwafikia Watoto yatima, wafungwa wakike, waathirika wadawa za kulevya n.k

Jumla ya paketi 150 za mchele na paketi 150 za unga wa mahindi zenye ujazowa kilo Zaidi ya 1500 viligawiwa.

MATUKIO KATIKA PICHA









Maswali kutoka katika kitabu cha

Makusudio 23 Adhimu ya ujenzi wa Baitullah

Ni muhimu , anayekariri au anayepitia asome kitabu angalau mara mbili na kuyatafuta majibu kutoka katika kitabu
(Atfal,Khudam na Nasirat wa Simiyu huwa wanahifadhi Maswali na majibu hayo na kufanya mashindano kila wiki)
Imetayarishwa na:
Sheikh Ali Dino Tahir – Simiyu

Uk.1, 2 1. Taja jina la mwandishi wa kitabu cha MAKUSUDIO 23 ADHIMU YA UJENZI WA BAITULLAH ? Jibu. Hadhrat Mirza Nasir Ahmad Khalifatul Masih wa tatu Radhiallahu Anhu

Uk. 3 2. Mungu alijenga upya Kaabatullah kupitia nani? Jibu. Nabii Ibrahim Alaih Salam

Uk. 4 3. Baitullahi ilijengewa upya kwa ajili ya nani. Jibu: Kwa ajili ya Nabii wa mwisho wa kuleta sheria

Uk. 6 4. Ni nani aliyejenga Kaabatullah mara ya kwanza Jibu: Nabii Adamu Alaih sallam

5. Nyumba gani ilijengwa kwa ufunuo. Jibu: Kaabatullah

Uk. 7 6.Nani alifanya ukarabati wa Kaabatullah? Nabii Ibrahim AS na Nabii Ismail AS

7. Kwanini Mungu alitaka kizazi cha Nabii Ibrahim Alaih Salam kuishi karibu na Kaabatullah?
Jibu: Ili izalike kaumu watakaohudumu nyumba ya Allah na alipokuja Mtume Muhammad SAW wakamsaidia kwa hali na mali

Uk. 8 8.Shabaha au Kusudio la kwanza la Baitullah ni nini?
Jibu:Ilivyotajwa katika Quran { وضع للناس } {Wudhi'a linnaas} yaani Kutoka humo mataifa yote ya dunia bila ya ubaguzi wa rangi na kimbari yapata manufaa ya dini na ya kidunia

9.Taja Majina mengine ya Baitullah ? Jibu: Kaabatullah,Baitullah , Kibla na khana kaaba.

Uk. 9 10. Shabaha au Kusudio la pili la Baitullah ni nini ?
Jibu: Kusudio la pili limeambiwa katika neno {Mubarakan} مبارکا kwamba Baitullah iwe inazuriwa kwa lengo la kuimarisha hapa sheria ,kumuinua hapa Nabii mwenye kuleta sheria ya mwisho ambayo ndani mwake miongozo yote na kweli zote za kiroho zijumuishwe zilizokuwa zikuwepo katika sheria tofauti za mataifa mbalimbali,na usibaki ukweli wowote nje ya sheria hii.

11. Maana ya Hudallil aalamiin ni nini? Jibu: Mwongozo kwa walimwengu wote

Uk.10 12.Kuhusu Baitullah yalikuja maneno ya Wudhi›a linnasi ,maana yake ni nini?
Jibu: tuwajengea nyumba hii kwa dunia nzima mataifa yote na zama zote.

13.Ubainishe maana ya ndani katika maneno ya Hudalil aalamiin yaani Mwongozo kwa walimwengu wote? Jibu: Hapo Mungu anakusudia kwamba mataifa yote ni sawa kiakili na kibusara na kielimu vina vipaji vya kuuelewa mwongozo huo vizuri na taifa moja halina ubora kuliko jingine.

Uk.11 14. Mungu aliposema kuhusu Sheria ya mwisho iliyokamilika ni kwa ajili ya wanadamu wote ,jambo hili linakanusha mambo gani ?
Jibu: Hapo Mwenyezi Mungu anawakanusha wale wasemao kwamba Sisi tunayo akili nyingi na kipawa zaidi cha kuelimisha kuliko wengine.

15. Tofauti kubwa kati ya manabii wengine wote na Nabii Muhammad saw ni nini?
Jibu: Kila Nabii kabla ya Mtume[saw] alitumwa kwa ajili ya zama zake na kabila au taifa lake tu na Mtume Muhammad SAW alitumwa kwa watu wote duniani mpaka Kiyama.

Uk.12 16.kuna tofauti gani kuhusu pepo baina ya Islam na dini zingine ?
Jibu: Dini zingine zinaamini watenda wema watapata pepo baada ya kifo lakini sawa na itikadi ya Islam zawadi ya pepo si katika Akhira tu bali mtenda wema hupewa pepo katika Maisha ya dunia hii pia.

Uk. 13 17. Kusudio la tatu la Baitullah ni nini ? Jibu: kama alivyosema Allah mtukufu هدی للعالمین {Hudan lil'aalamiin} Ili Baitullah iwe muongozo kwa walimwengu wote.

Uk. 14 18. Kusudio la nne la Baitullah ni nini ?
Jibu: Kama asemavyo Allah آیات بیینات {aayatim bayyinat} ili Ishara Bayana zitakazohusiana na nyumba hii na itakuwa chanzo cha ishara na misaada ya kimbingu zitakazodumu milele.

Uk. 15 19. Kusudio la tano la Baitullah ni nini ? Jibu: kama alivyosema Mungu مقام ابراهیم {makamu ibrahiim } ili tumuige mja wa Mungu Nabii Ibrahim Alaih salam na wazao wake ambao wakitengana na nafsi zao na kuzama ndani ya huba na mapenzi ya Mungu.

20. Kaulimbiu ya wanaoiga Nabii Ibrahim Alaih Salam ni nini?
Jibu: Aslamtu Lirabbil 'alamiin Yaani Nimejitupa kwa Mola wa walimwengu

21. Hadhrat Imam Mahdi Alaih Salam alitaja aina mbili za ibada uzitaje? Jibu: 1. Ibada inayoimarika juu ya misingi ya unyenyekevu 2. Inayoimarika juu ya misingi ya mahaba na kutokuwa na ubinafsi

22.Kamilisha sentensi: Yule aliye na kiburi sawa na chembe mbele ya Mola wake ..
Jibu: Yule aliye na kiburi sawa na chembe mbele ya Mola wake Dua yake haiwezi kupokelewa abadan.

Uk.16 23.Ni nani aliyetoa wazao wake wakfu kwa ajili ya Baitullah.
Jibu: Nabii Ibrahim Alaih Salam

24.Wakf maana yake nini?
Jibu:Kujitolea maisha kwa ajili ya kazi ya dini.

Uk.17 25. Kaumu au umma wa nani unaodumisha kumbukumbu ya Nabii Ibrahim AS ?
Jibu:Umma wa Mtume Muhammad swallalahu alaihi wasallam.

Uk.22 26.Nabii Ibrahim AS alimuomba sana Mola wake kuhusu kupatikana kaumu maalum watakaoimarisha Baitullah,ombi lake lilikubaliwa lini? Jibu: Baada ya miaka 2500 .
27. Ombi la Nabii Ibrahim[as] lilipokubaliwa baada ya Miaka 2500 ilitokea nini.?
Jibu: MTUME MUHAMMAD SAW ALITUMWA NA IKAPATIKANA KAUMU ILIYOKUWA NA NGUVU NA VIPAJI VYA KUBEBA MAJUKUMU MAZITO YA SHERIA KAMILIFU, TIMILIFU ILIYOKUWA KWA AJILI YA DUNIA NZIMA.

Uk. 23. 28.Kusudio la sita la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu:Kama Alivyosema Allah mtukufu من دخل کان آمنا Man dakhala kana Aamina yaani atakayeingia humo atakuwa na amani ya kila namna.

29.Atakayeingia humo yaani katika Kaabatullah atapata amani ,Maana yake nini ? Jibu: kila Atakayefanya zile ibada zihusianazo na Baitullah kwa nia halisi, mtu huyo atapata hifadhi ya Mungu na dhambi zake zitasamehewa.

Uk. 24. 30. Kusudio la saba la ujenzi wa Baitullah ni nini?
Jibu: وللہ علی الناس حج البیت Wa lillahi 'alannasi hijjul Baiti. Yaani ili watu wote duniani wajumuike sehemu hii kwa hija.

31. Hija ni nini? Jibu: Kuzuru Baitullah wakati husika na kufanya ibada zote alizozifanya Mtume Muhammad SAW ni hija.

32. Kusudio la nane la ujenzi wa Baitullah ni nini? Jibu: Kusudio la nane la ujenzi wa Baitullah limeelezwa katika neno {Muthabatan} مثابۃ hivyo imesemwa hapo kwamba ingawaje mifarakano ya dini itafikia kilele chake lakini ni utashi wa Mwenyezi Mungu kumtuma wakati ule Mtume Muhammad[saw] atakayefanya mataifa yote kuwa ummati mmoja.

Uk. 25. 33. Kusudio la tisa la ujenzi wa Baitullah ni nini?
Jibu: Kusudio la tisa la ujenzi wa Baitullah limeandikwa katika neno {Amnan} yaani Nyumba hii ni amani kwa watu

34. Je, Kaabatullah ni amani kwa watu ? Jibu: Dunia yaweza kupata amani ya kweli kwa kutekeleza mafundisho yale tu atakayoitolea yule Nabii atakayeinuliwa kutoka katika Baitullah na upande wa dunia ya kiroho utulivu wa moyo utapatikana kupitia yeye.

Uk. 26. 35. Kusudio la kumi la Jibu: ujenzi wa Baitullah ni nini?
iliyoandikwa katika aya
اتخذوا من مقام ابراهیم مصلی{Ittakhidhuu min makami ibrahma musalla} yaani iumbwe kaumu ambayo iwe inafanya ibada ya Mola wake kwa kujinyenyekeza sana na iimarishe duniani kote vivuli vya daraja la Hadhrat Ibrahim[as] kwa ajili ya ibada yenye unyenyekevu mkubwa.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Dhihirisho la majina ya Muhammad na Ahmad

Kutoka uk. 12

yeyote anaachana nanyi hivyo ndivyo nyinyi pia katika mwaka wowote mtaachana na marafiki zenu. Basi jitahadharini na sumu ya zama hizi baya isilete athari juu yenu. Rekebisheni sana hali zenu za huluka. Jiepusheni na chuki, bughuda na kiburi na onyesheni watu wa dunia miujiza ya kikhulka. Mmeshasikiliza kwamba Nabii wetu[saw] ana majina mawili: 1. Kwanza ni Muhammad saw, jina hili limeandikwa katika Torati iliyo sheria moto moto kama inavyodhihiri kwa aya hii:

مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ وَ الَّذِيْنَ مَعَهٗۤ اَشِدَّآءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ ... ذٰلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرٰىةِ

Yaani Muhammad ni Mtume wa Allah, na walio pamoja naye ni imara mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao; huu ndio mfano wao katika Taurati. (Al-Fath, 48/30)

2. Jina la pili ni Ahmad saw na jina hili lipo katika Injili iliyo mafundisho ya Mungu katika sura ya kijamali, kama vile ni dhahiri kwa aya hii:

وَ مُبَشِّرًا بِرَسُوْلٍ يَّاْتِيْ مِنْۢ بَعْدِي اسْمُهٗۤ اَحْمَدُ

Yaani Na kutoa habari njema ya Mtume atakayefika nyuma yangu jina lake ni Ahmad. (As-Saf, 61/7)

Na Nabii wetu ndiye mwenye kukusanya sifa zote mbili za jalali na jamali. Maisha ya Maka yalikuwa katika hali ya kijamali na maisha ya Madina katika hali ya kijalali. Kisha sifa hizi mbili zikaganwanyika kwa umati kwamba masahaba wakapewa maisha ya hali ya kijalali na kwa maisha ya hali ya kijamali Masihi Mauudi akafanywa mdhihirisho wa Mtume Mtukufu saw. Hiyo ni sababu kwamba ikasemwa kwake:[1] يضع الحربَ yaani hatapigana vita na hii ilikuwa ahadi ya Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu kwamba kwa kutimiza sehemu hii Masihi Mauudi na Jumuiya yake itadhihirishwa. Kama vile kuna ishara katika aya hii:

وَّ اٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوْا بِهِمْ

Yaani na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao. (Al-Jumua, 62/4)Na aya:

تَضَعَ الْحَرْبُ اَوْزَارَهَا

Yaani hata vita vitue mizigo yake. (Muhammad, 47/5). Basi sikilizeni kwa makini kwamba baada ya miaka elfu moja na mia tatu kwa kuonyesha mfano wa maisha ya aina ya kijamali nyinyi mmeumbwa. Huu ni mtihani kutoka kwa Mungu na yeye Anawajaribuni kwamba mko vipi katika kuonyesha mfano huu. Kabla yenu Masahaba ra mfano wa maisha ya kijalali kwa njia ya kusifiwa na wakati ule ukafaa kwamba mfano wa maisha ya kijalali ungeonyeshwa kwani waaminio wakauawa kama kondoo na mbuzi kwa kuheshimu masanamu na kusaidia ibada ya viumbe. Na mawe, nyota, vitu na viumbe vingine vikawekwa mahali pa Mungu.

Kwa hiyo bila shaka zama zile zilikuwa zama za jihadi ili watu ambao wanainua upanga wauawe kwa upanga tu. Basi Masahaba ra wakanyamazisha kwa upanga walioinua upanga na kwa kudhihirisha udhihirisho wa jina la Muhammad lililo dhihirisho la Ujalali na shani ya kupendwa wakaonyesha vizuri umahiri na kumwaga damo yao kwa kuhami dini.

Kisha baada yake waongo wakazaliwa ambao hawakuwa wadhihirishao wa ujalali wa jina la Muhammad bali wengi wao walikuwa kama waizi na wajambazi waliopita kabla yangu walioitwa Wamuhammadi kwa uongo na watu wakawaelewa kama wapendeleao; kama vile hata siku hizi pia baadhi ya wajinga wa mipakani wakidanganywa na mafundisho ya masheikh wa namna hii kwa udhuru wa kudhihirisha ujalali wa Kimuhammadi wanao njia ya wizi na mara kwa mara wanafanya mauaji bila haki. Lakini sikilizeni kwa umakini kwamba sasa sio wakati wa kudhihirisha dhihirisho la jina la Kimuhammadi yaani sasa haikubaki huduma yoyote ya aina ya ujalali. Kwani ujalai ule umeshadhihirika kwa kiwango cha kutosha. Haiwezi kustahimili miale ya jua tena. Sasa inahitajika nuru ya baridi ya mwezi na kwa njia ya Ahmad nuru ile ni mimi. Sasa ni wakati wa kudhihirisha mfano wa jina la Ahmad yaani ni siku za huduma za aina ya ujamali na ni zama za kudhihirisha ukamilifu wa maadili. Mtume wetu saw alikuwa mfano wa Musa as na mfano wa Isa as pia, Musa as akaja kwa rangi ya ujalali na akatawaliwa na rangi ya ujalali na ghadhabu ya Mungu lakini Isa as akaja kwa rangi ya ujamali na katawaliwa na unyenyekevu. Basi Nabii wetu saw akadhihirisha mifano hii mbili ya ujalali na ujamali katika maisha yake ya Maka na Madina. Kisha akataka kwamba baada yake, Jumuiya yake pia iliyofaidika naye walio warthi wake wa kiroho idhihirishe mifano hii mbili. Basi akaweka Masahaba ra kwa kudhihirisha mfano wa kijalali kwani katika zama zile kwa kudhulumiwa kwa Islam dawa hiyo ilikuwa sawa.

Kisha zama zile zikatoweka na hakubaki mtu yeyote ardhini kwamba adhulumu Islam kwa jina la dini. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu Akifuta rangi ya kijalali Akataka kudhihirisha mfano wa jina la Ahmad yaani kataka kudhihirisha rangi ya kijamali. Hivyo basi sawa na ahadi ya kale Akamwumba Masihi Mauudi wake aliye mfano wa Isa akiwa katika rangi ya Ahmadi na ni mwenye kudhihirisha hulka za kijamali na Mwenyezi Mungu Amewafanyeni kama viungo kwa Isa anaye sifa ya Ahmad. Basi sasa ni wakati kwamba mmonyeshe uzuri na ujamali wa nguvu za kikhulka. Inapaswa kwamba muwe na huruma kwa kiumbe cha Mungu wala usipatikane udanganyifu wowote katika tabia yenu. Nyinyi ni wadhihirisho wa jina la Ahmad kwa hiyo inapaswa kwamba usiku na mchana kazi yenu iwe kumhimidi na kumtukuza Mungu na hali ya utimishi inayolazimu kwa kuwa mwenye kuhimidi, iwekeni ndani mwenu.

Na hamwezi kumhimidi Mwenyezi Mungu kwa ukamilifu mpaka mmwone Mola wa walimwengu yaani Malezi wa dunia nzima. Na hamwezi kuwa wakweli katika kauli hii mpaka mmjifanyie pia kama Yeye kwani ikiwa unamsifu yeyote kwa sifa njema na mwenyewe unayo itikadi na khulka kinyume cha sifa hii basi kana kwamba unamfanyia mtu yule dhihaka kwamba ambacho hukipendi kwa ajili yako unakijuzu kwake ilihali Mola wako Ameanzia Neno lake kwa ربُّ العالمين yaani Mola wa walimwengu, Anawafaidisha wote wema na wabaya kwa vitu vyote vya kula vya ardhi, hewa yote ya angaa, nyota za mbinguni na kwa jua na mwezi wake basi inapaswa iwe faradhi yenu kwamba hulka hii iwe ndani mwenu pia waila hamwezi kuitwa *Ahmad* na *Hamid* yaani mwenye kuhimidi kwani *Ahmad* ni yule anayemhimidi sana Mwenyezi Mungu. Na mtu ambaye anayemsifu sana yeyote hupenda hulka zile zile kwa ajili yake alizonazo na hutaka kwamba hulka zile ziwe ndani mwake. Basi mtawezaje kuwa *Ahmad* na *Hamid* wa kweli ilihali hampendi hulka hizi kwa ajili yenu. Kwa kweli muwe Ahmadi na mmelewe kwa yakini kwamba Mwenyezi Mungu anazo sifa nne tu za asili na za hulka zilizoelezwa katika Suratul Fatiha. 1. *Rabbul Aalamiin* yaani Mlezi wa walimwengu. 2. Rahmani yaani Mwenye kurehemu bila huduma yoyote. 3. Rahimu yaani Mwenye kuzawadia zaidi ya haki na Mwenye kukubali huduma na asiyeipoteza. 4. Mwadilifu wa waja wake.

Basi Ahmad ni yule ambaye anayekusanya ndani yake sifa hizi nne kwa namna ya kivuli. Hiyo ni sababu kwamba jina la Ahmad ni dhihirisho la jamali na kinyume chake jina la Muhammad ni dhihirisho la jalali.

Sababu yake ni hii kwamba katika jina la Muhammad kuna siri ya kupendwa kwani ni mwenye kukusanya sifa na uzuri wa daraja ya ukamilifu na kuwa mwenye kukusanya sifa hutaka ujalali na ukubwa. Lakini katika jina la Ahmad kuna siri ya kupenda kwani kusifu kunalazimu unyenyekevu wa aina aina, hiyo inaitwa hali ya ujamali na hali hii inahitaji unyenyekevu. Katika Nabii wetu saw ilikuwa shani ya kupendwa pia inayolazimu jina la Muhammad kwani kuwa Muhammad yaani kuwa mwenye sifa zote kunazalisha shani ya kupendwa. Na katika dhati ya Mtume Mtukufu saw ilikuwa shani ya kupenda pia inayolazimu jina la Ahmad kwani ni lazima msifu awe mpenda. Kila mtu anamsifu yeyote sifa ya kweli na ya ukamilifu anapokuwa mpenda wake bali awe aashiki wake. Na kwa kuwa mpenda unyenyekevu ni lazima na hiyo ni hali ya ujamali inayolazimu hakika ya Ahmadiyya.

Kupendwa kuliyofichika katika jina la Muhammad kulidhihirika kupitia Masahaba. Na watukanaji waliopaswa kupigwa, ujalali wa kuwa mpendwa wa Mungu uliwapiga lakini katika jina la Ahmad kulikuwa shani ya kupenda yaani unyenyekevu wa kiaashiki, shani hii ikadhihirika kwa kupitia Masihi Mauudi. Basi nyinyi ni wadhihirishao wa shani ya Uahmadiyya. Kwa hiyo malizeni kila jazba yenu isiyofaa na onyesheni unenyekevu wa kiashiki. Mwenyezi Mungu Awe nanyi. Aamin ***(Arobaini uk.13-17)***

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania


MapenziyaMungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Kuelekea Ijtimaa ya Kitaifa Lajna Imaillah

UK. 03






Buriani Muhammad Iqbar Dar

BURIANI MOHAMMED IQBAL DAR SAHIB

Na. Mahmood Hamsin Mubiru



Ni saa kumi na moja na dakika ishirini na moja, siku ya kwanza ya mwezi mtukufu wa Ramadhani jumapili tarehe 02/03/2025. Mjukuu wangu ameambiwa aniletee simu yangu. Nilikuwa uani nikisoma. Kabla hajafika simu inakata. Natizama aliyenipigia ni Maulana Alhaji Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya. Haraka nachukua simu na kumpigia, nampata tunapeana Assalaam Alaikum na ananiambia ***'Innaalillaahir wa inna ilaihi Raajiuun'*** Ndugu yetu Mohammed Iqbar Dar ametutoka. Ananieleza kuwa habari hizi zimetolewa na Naib Amir na Mkuu wa Chuo cha Jamia Morogoro, Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib. Namshukuru kwa taarifa na kabla sijaweka simu chini, chozi linanidondoka.

HABARI UK> 04



Dhihirisho la majina ya Muhammad na Ahmad


Na
Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani Sahib

Seyidna Ahmad as. Masihi Mauudi na Mahdi wa ahadi akiwasihi na kuwaelimisha wapendwa wake amesema kwamba Enyi wapendwa, mmepata zama ambazo manabii wote walizibashiria na mmemwona mtu yule yaani Masihi Mauudi ambaye mitume kadhaa pia walitamani kumwona. Kwa hiyo sasa imarisheni sana imani yenu na rekebisheni njia zenu, takaseni mioyo yenu na mridhishe Mola wenu.

Enyi marafiki, mpo katika nyumba ya safari yaani duniani



kwa siku chache tu, kumbukeni nyumba zenu hasa. Mnaona kwamba kila mwaka rafiki



True Justice and Peace
Concluding Address
(Swahili Translation)

This is the concluding address delivered by Hazrat Khalifatul-Masīḥ V (may Allah be his Helper), at the Annual Convention of the Ahmadiyya Muslim Community United Kingdom in 2015. In this address Huzoor speaks of the various causes that have resulted in increased turmoil throughout the world. He rightly points out that the conflict that has emerged throughout the world is one which relates to all the nations of the world and no nation, whether third world or not, is free from the grips of unrest. He states that the reason the world continues to suffer is because it has forgotten God, who is the creator of all. No progress or success can be attained without God. Islam is a religion of peace and if its true teachings are followed, the disorder that is seen to exist in the world today would vanish.
Huzoor states that the only way the people of the world can be alleviated from the clutches of conflict is by recognising God, establishing unconditional justice in the world, and by showing true sympathy to mankind.

ISBN 1848805460

Uadilifu wa Kweli na Amani

na

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad

Imamu na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waamadiyya Duniani, Khalifa wa Tano wa Masihi Mau'udi[as],
(Allah Awe Msaidizi wake)

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA
TANZANIA

Je, Wajua?

Jonny Kim ni Luteni Kamanda wa Jeshi la Wanamaji la Marekani, aliyekuwa Navy SEAL, daktari (M.D. kutoka Shule ya Matibabu ya Harvard), naval aviator, na astronaut wa NASA.

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 2,300/=.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com